

I Idara ya Elimu ya NSW

Matazamio ya salama ya COVID-19 safe wakati wa mitihani ya mwandiko ya HSC

Habari hii itasaidia wanafunzi kuelewa mipangilio salama ya COVID-19 safe wakati wa kuhudhuria mitihani wao wa HSC. Usalama na ustawi wa wanafunzi na wafanyakazi ambao wanahudhuria ni muhimu sana kwetu na kwa hivyo tunawaomba wanafunzi wote kushirikiana na mipangilio hii wakati wote.

Uchunguzi kwa wanafunzi wanazo dalili

- Wanafunzi hawapaswi kuhudhuria mitihani ikiwa wanajisikia wagonjwa
- Wanafunzi wataulizwa baada ya kuwasili ikiwa wana dalili kama za homa ya mafua (flu) au ikiwa wanapaswa kujitenga chini ya uongozi wa NSW Health (Idara ya Afya ya NSW)
- Wanafunzi wanaonyesha dalili kama za homa ya mafua au ambao wanashauri kuwa wanaumwa wataombwa kuondoka shuleni na kupanga kupimwa kwa COVID-19
- Wanafunzi walio na historia ya matibabu au ugonjwa unaojulikana ambao unaweza kuonekana kama dalili za COVID-19 wanapaswa kupanga sasa na kuzungumza na daktari wao (GP). GP anaweza kutoa hakikisho la mwandiko - k.m. mwanafunzi anaonyesha dalili hii kwa kawaida.

Dalili kama za homa ya mafua

Dalili kama za homa ya mafua ni pamoja na homa, kikohozi, maumivu ya koo, upungufu wa pumzi, kupoteza ladha, na kupoteza harufu. Taarifa ya ziada kuhusu dalili za COVID-19 zinaweza kupatikana kwenye tovuti ya Afya ya NSW, [NSW Health website](#).

Wanafunzi ambao wanaonyesha hata dalili dhaifu kama za homa ya mafua (flu) wanapaswa kuondoka mara moja na wasirudi mpaka watakapokuwa wamepimwa hasi wa COVID-19 na hawana dalili.

Kufuatilia haraka majibu ya kipimo cha COVID-19

Wanafunzi wa HSC wanaweza kufuatilia haraka majibu yao ya kipimo cha COVID-19.

Kufanya hivi wanapaswa:

- kusema yeye ni mwanafunzi wa HSC wakati anapopimwa
- kuhakikisha muuguzi au daktari anayefanya kipimo anaandika pendekezo yake 'haraka — HSC'
- kujitenga hadi jibu ya hasi yatapokelewa
- kuonyesha shule yake matokeo ya hasi (yaani hana COVID-19)
- piga simu kwa nambari ya mawasiliano inayotolewa na kliniki kama majibu hayajapokewa katika masaa 36.

Kupunguza hatari ya kusambaza

- Wanafunzi wanapaswa kuosha mikono yao au kutumia sanitaiza ya mikono kabla ya kuanza mtihani.
- Endeleza mazoea mazuri ya usafi wakati wa mtihani ikiwa ni pamoja na kuzuia kikohozi au kupiga chafya kwa kukohoa au kupiga chafya kwenye kiwiko chao au tishu, kutupa tishu mwishoni mwa mtihani
- Epuka kupeana mikono au kumbatiana wanafunzi wengine siku ya mitihani.
- Vifaa vya usafi ambavyo vitapatikana katika mahali pote pa mtihani ni:
 - Sanitaiza
 - Vifuto
- Mwanafunzi anaweza kusafisha kwa kufuta meza yake kabla ya kuanza mtihani wake ikiwa atachagua kufanya hivyo.
- Wanafunzi wasichanganyike katika vikundi vikubwa kabla au baada ya mtihani.
- Vyumba vya mtihani vitasafishwa kila siku.

Mipangilio ya kufika na kusaini

- Wanafunzi wanapaswa kufika sio zaidi ya dakika 20 kabla ya mtihani na kuripoti moja kwa moja kwenye chumba cha mtihani kilichoteuliwa kwa uchunguzi na kusaini.
- Wanafunzi wataombwa kusaini karatasi ya mahudhurio inayothibitisha kuhudhuria mtihani, kutoa maelezo ya mawasiliano na kwamba hawana dalili kama za homa ya mafua.

Maeneo mbadala ya mtihani

Shule yako imetambua eneo mbadala la mtihani iwapo mtihani hauwezi kuendelea katika eneo lililopangwa. Habari hii itapewa kwako kwenye ratiba yako ya kibinafsi cha mtihani kwa hivyo inapatikana kwa haraka kwa taarifa fupi ikiwa itahitajika.

Hii ni kwa dharura tu na wanafunzi wanapaswa kuhudhuria eneo lililopangwa ila kama wanashauriwa na shule. Usihudhurie eneo mbadala lililopendekezwa kama hujaambiwa ufanye hivyo na shule.

Kesi zilizothibitishwa za COVID-19

Kama, wakati wa kipindi cha mtihani, shule inashauriwa na NSW Health kwamba kumekuwa na kesi iliyothibitishwa ya COVID-19 ambayo itaathiri shule, mipangilio ipo ili kupunguza usumbufu inapowezekana. Shule inaweza kukushauri siku moja kabla kwamba mtihani utahamishiwa kwa eneo mbadala lililoelezewa katika ratiba yako au mtihani unaweza kufutwa.

Ugonjwa/Bahati mbaya

Wanafunzi ambao hawahudhuri mtihani kwa sababu ya kuwa na dalili, au ambao wamekataliwa kwa sababu ya uchunguzi watastahiki madai ya ugonjwa/ bahati mbaya. Shule yako itakusaidia kupitia mchakato huu inapohitajika.

Huduma ya Ukalimani wa Simu

Ikiwa unahitaji habari zaidi tafadhali piga simu kwa mwalimu mkuu wa shule yako. Ikiwa unahitaji mkalimani kukusaidia kwa maswali yako tafadhali piga simu kwa Huduma ya Ukalimani wa Simu kwenye 131 450 na uombe mkalimani kwa lugha yako. Huduma hii itakuwa ya bure kwako.